# JARIDA LA ACT
## TOLEO NA.45 (Jan - Mach 2032)
## Tunaunganisha, Shawishi na Kutetea

### *Wajumbe wa Bodi*

Dkt. Jacqueline Mkindi

**Mwenyekiti**

Mhe. Jitu Soni- Makamu/Mkt

Dkt. Sinare Y. Sinare - Mjumbe

Bw. Fabian Mwakatuma - Mjumbe

Bw. Enock Ndodole - Mjumbe

Bw. Zubery Mwachulla- Mjumbe

Bw. Omary Mwaimu - Mjumbe

Bw. Joeseph Masimba - Mjumbe

Bibi. Elde Kimaro - Mjumbe

Bw. Abel Lyimo – Mjumbe

### *Yaliyomo*


Jukwaa la Biashara Lafanyika

Mjadala wa Kodi wa Kitaifa

ACT/BAYER- Watanua Wigo wa Mashirikiano

Mafunzo ya Mbinu Bora za Kilimo

Programu ya Kuwajengea Uwezo Vijana

Ziara ya EAFF Tanzania

Ziara ya Mafunzo, Zambia

Programu ya Kilimo Biashara kwa Vijana


## Makamu wa Rais, Akiwa kwenye Kongamano la Kibiashara baina ya Umoja wa Ulaya na Tanzania




## TUKIO LIJALO

Warsha ya Kisera ya Kitaifa **(AAPC**) – Dodoma, Tanzania

**Aprili 13 na 14, 2023**

**NANE NANE**; **Kitaifa -Mbeya**, Viwanja vya John Mwakangale

**Agosti 1 - 8, 2023**

Kongamano la Mifumo ya Chakula (**AGRF- Africa Food System Summit),** Dar es Salaam- Tanzania

**Septemba 5 - 8, 2013**

# JUKWAA LA KIBIASHARA LAFANYIKA – EU-TZ BUSINESS FORUM

Februari 23 na 24 2023, Ubalozi wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania kwa kushirikiana na wabia wake waliandaa kongamano la kwanza la kibiashara baina ya Umoja wa Ulaya na Tanzania (EU-TZ Business Forum). Kongamano hilo la siku mbili, lilifanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam. Jukwaa hilo la kibiashara liliandaliwa kwa lengo kukuza biashara na uwekezaji baina ya nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya (EU) na Tanzania. Kongamano hilo la ngazi ya juu liliwaleta pamoja wadau mashuhuri wa biashara na uwekezaji kutoka Umoja wa Ulaya na Tanzania. Makamu wa Rais Dk. Philipo I. Mpango alifungua jukwaa hilo kwa kuwahakikishia wawekezaji kuhusu dhamira ya Tanzania katika kuboresha mazingira ya biashara kwa wawekezaji.




***Makamu wa Rais Dkt. Philipo I. Mpango, akifungua jukwaa la kibiashara baina ya Umoja wa Ulaya na Tanzania lililofanyika Dar es Salaam.***

Kongamano hilo liliwakutanisha pamoja waonyeshaji zaidi 400 na washiriki 700 kutoka Tanzania Bara, Zanzibar na Umoja wa Ulaya. Tanzania Kama kitovu cha uwekezaji, fursa na faida linganishi ni miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa wakati wa kongamano. Jukwaa hilo pia lilitoa fursa baina ya Sekta Binafsi na Umma kujadili namna ya kuboresha mazingira ya kibiashara kama vile mpango wa Serikali kutatua changamoto za kibiashara (regulatory framework), kufanya mikutano ya kibiashara na makongamano ya kibiashara baina ya Tanzania na Umoja wa Ulaya. Taasisi ya Sekta Binafsi Nchini (TPSF), Baraza la Kilimo (ACT), Chama cha Wakulima wa Matunda na Mboga mboga (TAHA), Shirikisho la Watu wenye Viwanda Tanzania (CTI), Chamba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA), Chemba ya Wanawake Wafanyabiashara (TWCC) walikuwa sehemu ya kamati ya maandalizi, huku sekta ya umma ikiwakilishwa na Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), Wizara ya Kilimo (MoA), Wizara ya Mifugo na Uvuvi (MLF) n.k... ACT iliwakilishwa na Bw. Timoth Mmbaga (Mkurugenzi Mtendaji), Mwenyekiti, Dkt. Jacqueline Mkindi, na wanachama wake.



# MJADALA WA KODI WA KITAIFA

Januari 21, 2023, Wizara ya Fedha na Mipango iliendesha mjadala wa Kitaifa kuhusu masuala yanayohusiana na kodi uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam. Mjadala wa kitaifa ulipambwa na kaulimbiu isemayo, **"*Marekebisho ya Sera kwa Maendeleo*"** na kuwakutanisha pamoja watendaji wakuu wa sekta za umma na binafsi kama vile Taasisi ya Sekta Binafsi Nchini (TPSF), Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI), Shirikisho la Utalii Tanzania (TCT), Baraza la Kilimo Tanzania (ACT), Chama cha Mboga mboga na Matunda (TAHA), Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) na jumuiya za wafanyabiashara nchini. Mgeni Rasmi alikuwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye alisisitiza ahadi za Serikali katika kuweka sera bora na rafiki katika usimamizi wa kodi unaozingatia ulipaji na kuongeza pato. Dkt. Nchemba alisema "*Kuna uhusiano wa karibu sana kati ya sera nzuri za kikodi kwa upande mmoja na ukuaji wa biashara na maendeleo ya nchi kwa upande mwingine*."



***Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Nchemba akifafanua jambo wakati wa mjadala wa kodi wa kitaifa uliofanyika Dar es Salaam***

Waziri wa Fedha, Dkt. Nchemba; "*Rais Samia Suluhu Hassan ametuagiza mara kadhaa tuendelee kuboresha sera zetu za kodi kwa kuingiza maoni kutoka kwa wadau kupitia midahalo kama hii ya kikodi."* Pia alifafanua nia ya kutumia makusanyo kukuza biashara ili kuiwezesha Serikali kukusanya kodi zaidi. Alielezea umuhimu wa kupanua wigo wa kodi ili kupunguza mzigo unaobebwa na walipakodi wachache wanaotambulika (formal business). Kupitia mjadala huo, Dkt Nchemba alisisitiza umuhimu wa kuwa na Sekta binafsi imara itakayochangia kutoa ajira na kuongeza mapato kwa Serikali. Mjadala huo, ulibainisha umuhimu wa Serikali na Sekta binafsi kushirikiana katika kuweka mifumo madhubuti ya ulipaji kodi kwa hiari. Jumuiya ya wafanyabiashara nchini ilipata nafasi ya kujadili masuala kadhaa yanayohusiana na kodi ambayo wanatamani Serikali ifanyie kazi katika jitihada za kuboresha mazingira ya kibiashara kwa lengo la kukuza uchumi.

# ACT/BAYAER WATANUA WIGO WA MASHIRIKIANO

Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) kwa kushirikiana na kampuni ya kimataifa ya BAYER wanatekeleza mradi wa pamoja ujilikanao kama ***“Mradi wa Shamba Darasa”.*** Msimu wa kilimo 2022/23, mradi huu wa ubia umejikita katika kuhamasisha matumizi ya pembejeo za kilimo katika wilaya 14 za Tanzania Bara (Wanging'ombe, Ludewa, Songea, Mbinga, Hai, Siha, Monduli, Arumeru, Moshi, Babati, Kiteto, Kondoa, Kilindi na Handeni). Kwa ujumla, mradi umelenga kuwafikia wakulima wadogo 90,300 kwa kuwapatia mbinu bora za kilimo, huduma za ugani na kuendesha majukwaa ya kibiashara (B2B) sambamba na kuwa na “*Siku ya Wakulima”* (Farmers Field Day). Mradi huu ni matokeo ya utekelezaji mzuri wa mradi wa awali uliofahamika kama "*Better Farm Better Lives- BFBL)"*, uliohitimishwa Julai 2021 kwa mafanikio makubwa na kuweza kuwafikia wakulima wadogo takribani 115,000 katika wilaya 29.

Mradi wa shamba Darasa unalenga kuongeza uzalishaji na tija kwa wakulima wadogo kupitia matumizi sahihi ya teknolojia za kisasa kwenye kilimo. Mradi huu, unalenga kutoa mafunzo kwa washauri wa kilimo vijijini (VBA) 4, wafanyabiashara wa pembejeo (agro-dealers) 5 na wakulima viongozi (lead farmers) 150 (hadi 180) ambao watasaidia kufikia angalau wakulima wadogo 5,250 (na wasiozidi 6,300) kwa kila wilaya. Mradi utashirikisha wadau wengine kama vile: wadau/wafanyabiashara katika mnyororo wa thamani wa mahindi, Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ngazi ya wilaya/kijiji na makampuni yanayozalisha na kusambaza pembejeo.

Kuanzia Januari 3 mpaka 11, Sekretarieti ya ACT ikiongozwa na Bw. Mark Magila walitambulisha mradi katika wilaya 14 na kufanikiwa kukutana na Maafisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya (DALDOs) na Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya (DEDs). Kila wilaya imeteua Afisa Mazao ambaye atasimamia na kuratibu mawasiliano katika ngazi ya wilaya yanayohusiana na utekelezaji a mradi. Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) itakuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa mradi, wakati kampuni ya BAYER wanajukumu la kutoa pembejeo na fedha.



*Mkurugenzi wa Miradi kutoka ACT (Bw. Mark Magila- kushoto), Mratibu wa kanda (Bw. Richard Masandika- kulia) wakiwa na Bw. Kabula, (DALFO) wakati wa kutambulisha mradi Wilaya ya Monduli*



*Sekretariet ya ACT na mratibu wa kanda (Bw. Stephano Msuya) kutoka MVIWAKI, wakiwa na Bibi. Bertha Urio, Afisa Kilimo Wilaya (DAICO) wakati wa kutambulisha mradi wilaya ya Moshi vijijini*

# MAFUNZO YA MBINU BORA ZA KILIMO

Kuanzia Februari 19 hadi Machi 23 2023, ACT iliendesha mafunzo kuhusu mbinu bora za kilimo na matumizi sahihi ya viwatilifu kwa wakulima viongozi (lead farmers), wakala wa pembejeo (agro-dealers) na washauri wa kilimo vijijini (VBA) katika wilaya kumi na nne (14): Wangi'ngombe, Ludewa, Songea, Mbinga, Moshi, Hai, Siha, Babati, Meru, Kiteto, Kondoa, Monduli, Handeni na Kilindi. Mafunzo yaliendeshwa na Sekretarieti ya ACT (Bw. Khalid Ngassa, Bw. Obed Abraham, Bi. Agnes Ngondo, Bibi. Susan Masagasi, na Bi. Avelina Kuliwabu) kwa kushirikiana na waratibu wa kanda: Bi. Mwajuma Sizya (**Njombe**- Wangingo’mbe & Ludewa), Bw. Enock Ndunguru (**Ruvuma**-Songea na Mbinga vijijini), Bw. Edgar Lyakurwa (**Manyara** -Kiteto & Babati na **Dodoma**-Kondoa), Bw. Richard Masandika (**Arusha**-Monduli & Meru)  Bw. Stephano Msuya (**Moshi**-Siha, Moshi vijijini & Hai) na Bw. Seif Sempanga (**Tanga**- Kilindi & Handeni). Mafunzo yalifunguliwa na Bw. Khalid Ngassa (Meneja Huduma Uanachama) na Bw. Obed Abraham (Afisa Mradi) ambao walitoa maelezo mafupi kuhusu mradi na kuchagiza matumizi ya bidhaa zinazozalishwa na kampuni ya BAYER.



***Bw. Khalid Ngassa akitoa maelezo kuhusu mradi wakati wa mafunzo wilayani Babati***



***Bw. Thomas Magamba, akijibu hoja zilizowasilishwa na washiriki wakati wa mafunzo wilayani Kiteto***

Lengo kuu la mafunzo ni kupanua uelewa juu ya bidhaa zinazozalishwa na kampuni ya BAYER (pembejeo na viwatilifu). Mafunzo yaligusa mada zifuatazo i.) namna bora ya kutayarisha shamba ii) utambuzi wa mbegu bora na upandaji, iii) matumizi sahihi ya mbolea iv) matumizi sahihi ya viwatilifu (kiua gugu, wadudu nk) na v) namna bora ya kuhifadhi mazao baada ya mavuno.  Jumla ya washiriki 577 kati ya 660 walihudhuria mafunzo, sawa na asilimia 87.4. Mbali na mafunzo, ujumbe wa Sekretariet ya ACT ulitembelea mashamba darasa yaliyoandaliwa kama sehemu ya mafunzo. Jumla ya mashamba darasa 16 yalitembelewa kwa lengo la kuona namna yanavyoendeshwa na kusimamiwa na washauri wa kilimo vijijini (VBA) kulingana na mafunzo waliyopatiwa.




***Washiriki wa mafunzo wakiwa kwenye picha ya pamoja wilayani Meru.***




***Washiriki wa mafunzo wakiwa kwenye picha ya pamoja wilaya ya Songea vijijini.***



***Bw. Alfred Michael Haule (akiwa shamba), mkulima kiongozi kutoka kijiji cha Mkako, wilaya ya Mbinga: aina ya mbegu aliyopanda ni DK 777***



***Bw. Charles Osmand Ngonyani (akiwa shamba), mkulima kiongozi kutoka kijiji cha Lyagwene, wilaya ya Songea vijijini: aina ya mbegu aliyopanda ni DK 777***

# PROGRAMU YA KUWAJENGEA UWEZO VIJANA

Shirikisho la Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU) kwa kushirikiana na Andreas Hermes Akademie (AHA-International) wanaendesha ***"Programu ya Kuwajengea Uwezo Vijana"*** kwa nchi wanachama wa SADC. Tangu kuanzishwa kwa programu hii mwaka 2022, takribani washiriki 20 wamenufaika. Lengo kuu la programu ni kukuza uwezo wa kujitegemea miongoni mwa wakulima vijana kwa kuwapatia mafunzo yatakayowajenga na kuongeza ufanisi kwenye shughuli zao. Awamu ya pili ya programu (Cohort 2) ilikutanisha washiriki 19 kutoka nchi 8; Tanzania, Lesotho, E-swatini, Botswana, Namibia, Malawi. Madagaska na Zimbabwe. Mafunzo hayo ya ngazi ya juu ya uonozi yanatolewa katika muundo mseto (darasani na njia ya masafa-mtandao), yamegawanywa katika moduli mbili. Moduli ya kwanza ilitolewa Februari 21 hadi 28 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kopanong, Johannesburg - Afrika kusini ambapo washiriki walipata fursa ya kubadilishana uzoefu na wenzao kutoka Ujerumani ambao ni sehemu ya mafunzo hayo. Pia walipata nafasi ya kujifunza kutoka kwa Rais wa zamani wa Shirikisho la Wakulima Afrika (PAFO), Dkt. Theo De Jager ambaye aliwashauri kushiriki kikamilfu katika kusukuma ajenda ya kilimo na kuwa sehemu ya kushauri maboresho ya sera (policy reforms).  Aprili 24 mpaka Mei 1 2023, awamu ya pili ya mafunzo (module 2) itatolewa. Tanzania iliwakilishwa na Bw. Sospeter Mtenda kutoka kampuni ya kusindika na kuuza mchele ya Mtenda Kyela Rice Supply iliyopo Mbeya na Bw. Gabriel Mlay kutoka kampuni inayojishughulisha na uzalishaji na uuzaji wakuku na bidhaa zake maarufu kama VONKAVY COMPANY LIMITED iliyopo Morogoro.




*Washiriki wa Programu wakiwa kwenye picha ya pamoja, Johannesburg, South Africa*



## ZIARA YA EAFF TANZANIA

Tarehe 9 Februari 2023, Shirikisho la Wakulima wa Afrika Mashariki (EAFF) liliendesha warsha ya siku moja katika Hoteli ya Seychelles iliyopo Dar es Salaam, Tanzania. Warsha hiyo ilihudhuriwa na Wakurugenzi wa Bodi na Sekretarieti ya ACT na ilifunguliwa na Rais wa Shirikisho la Wakulima Afrika (PAFO) na Shirikisho la Wakulima wa Afrika Mashariki (EAFF) Bi. Elizabeth Nsimadala. Katika hotuba yake ya ufunguzi alitoa wito kwa wanachama wa EAFF kuanza kutoa huduma zinazoendana na mahitaji ya wanachama wake (wakulima na wafanyabiashara) ukanda wa Afrika Mashariki.



***Rais wa PAFO na EAFF, Bi.Elizabeth Nsimadala akiongea wakati wa ufunguzi wa warsha - Dar es Salaam.***

Warsha hiyo ilelenga kujadili na kutathimini uwezo wa taasisi kiutendaji (Organization Capacity Assesment-OCA) kwa taasisi wanachama wa EAFF nchini Tanzania ambazo ni ACT, TFC, MVIWATA na CUZA kutoka Zanzibar. Warsha hiyo ilitumika kama sehemu ya kuandaa mkakati wa pamoja wa kutoa huduma na kutetea maslahi ya wakulima katika ngazi ya kitaifa na kikanda (Jumuiya ya Afrika Mashariki).

.



***Washiriki wa warsha ya OCA wakiwa kwenye picha ya pamoja***

# ZIARA YA MAFUNZO, ZAMBIA

Andreas Hermes Akademie (AHA International) kwa kushirikiana na Shirikisho la Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU) waliandaa ziara ya mafunzo nchini Zambia (Wilaya ya Lusaka na Katete) kuanzia tarehe 5 hadi 12 Machi 2023 kwa nchi wanachama wa SACAU (Malawi, Lesotho, Zimbabwe, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Seychelles, Namibia, E-swatin, Tanzania, na Afrika Kusini). Mafunzo hayo ni muendelezo wa ziara iliyofanyika Ujerumani Oktoba mwaka jana; ziara ya Zambia ililenga kuwajengea uwezo wanachama (COP members) kupata maarifa na ujuzi kwa kujifunza kutoka kwa wakulima na wataalam kuhusu masuala yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi, na mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya haliyahewa. Kwa kifupi, ziara iliandaliwa kushughulikia mahitaji na kukuza uwezo wa wanachama kwa kuwapa mikakati ya kuendeleza mashirika ya wakulima na, kutatua changamoto za mabadiliko ya tabia nchi kwa lengo kuchochea kilimo endelevu na chenye tija. ACT ikiwa mwanachama (COP member), iliwakilishwa na Bi. Avelina Bernard - Afisa Sera. Bi. Avelina alipata nafasi ya kutembelea vituo vya kilimo kwa lengo la kujifunza; Kituo cha Maarifa na Mafunzo ya Kilimo (AKTC) mjini Lusaka na baadaye alitembelea Kituo cha Mafunzo kwa Wakulima (FTC) katika wilaya ya Katete, kaskazini-magharibi mwa Zambia.



*Bw. Helmut Anschuetz kutoka kituo cha kilimo cha AKTC, akiwa anatoa maelezo kwa wajumbe wa COP wakati wa Ziara Zambia*



***Wajumbe (COP members) wakiwa mashambani (field) kujifunza mazao himilivu wakati wa ukame (mabadiliko ya tabianchi)***

# PROGRAMU YA USTAWI WA BIASHARA YA KILIMO

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeanzisha ***Program ya Ajira kwa Vijana kupitia Sekta ya Kilimo*** kwa lengo la kutatua changamoto wanazo kutananazo vijana na wanawake katika sekta ya kilimo. Tangu kuzinduliwa kwa programu hii na Waziri Mkuu Mhe.Kassim M. Kassim Agosti 3, 2022 katika Maonesho ya Siku ya Wakulima maarufu kama Nane Nane yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya, mpango huo umevutia vijana kuchangamkia fursa zilizopo kwenye sekta ya kilimo. Wizara ya Kilimo (MoA) imetenga takribani ekari 162,492 kwa ajili ya shughuli za kilimo kupitia programu ya mashamba ya pamoja (block farms) katika mikoa ya Mbeya (Chunya), Dodoma (Chamwino), Kagera (Misenye) na Kigoma (Uvinza). Kupitia programu hii, ajira hadi millioni moja zitazalishwa, wakati sekta ya kilimo ikitarajiwa kukua kwa asilima 10 ifikapo mwaka 2030 (Ajenda10/30).

Lengo la jumla la Program ya Ajira kwa Vijana kupitia Sekta ya Kilimo ni kuimarisha ushiriki wa vijana katika sekta ya kilimo kwa ajili ya kilimo endelevu na kuboresha kipato. Malengo ya kimkakati ya BBT-YIA ni pamoja na: i) kuhamasisha vijana kuwa na mtazamo chanya juu ya kilimo kupitia mawasiliano ya kimkakati; ii) kuwezesha vijana kupitia wataalam elezekezi na washauri (mentoring and coaching); iii) kushirikisha vijana katika usimamizi wa biashara endelevu na zinazotengeneza faida; iv) kuweka mazingira wezeshi kwa kilimo biashara; na v) kuratibu na kuunganisha biashara za vijana kwenye mnyororo wathamani wa kilimo.

Vijana waliochaguliwa awamu ya kwanza ni 812 kati ya 20,227, sawa na asilimia 4 tu ndo waliopata nafasi ya kujifunza kwa vitendo kwa kipindi cha miezi minne kuanzia tarehe 17 Machi katika vituo atamizi 15 kikiwemo kituo cha mafunzo ya kilimo cha Bihawana mkoani Dodoma. Baada ya kuhitimu mafunzo hayo, vijana watapangiwa vituo vya kujifunza kwa vitendo kulingana na sifa na uhitaji. Programu hii inatazamwa kama mkombozi wa ajira kwa vijana, inakadiriwa biashara mpya 12,000 zitaanzishwa ndani ya kipindi cha miaka minane. Ili kutimiza azma hii, ubia/mashirikiano yanahitajika kati ya Wizara ya Kilimo na taasisi zifuatazo: Sekta binafsi, Wabia wa Maendeleo (Development Partners), Vyama vya Vijana katika Kilimo (Youth Associations) na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs).

Picha za vijana wakipatiwa mafunzo kwenye program ya BBT






TADB
"The Farmers' Bank"



## Dira na Dhamira

**DIRA**

Kuwa na sekta ya kilimo iliofanikiwa, endelevu na shindani inayohakikisha usalama wa chakula na lishe unaotokana na msukumo wa kisekta binafsi.

**DHAMIRA**

Kutetea, kuratibu na kuwezesha mazingira rafiki kwa kilimo-biashara.

## Bodi ya Uhariri

*1. Bw. Timoth Mmbaga - Mwenyekiti*

*2. Bw. Mark Magila - Mjumbe*

*3. Bibi. Laetitia William - Mjumbe*

*4. Bw. Khalid Ngassa - Mjumbe*

*5. Bibi. Susan Masagasi - Mjumbe*

**Wasiliana Na.**

Mkurugenzi Mtendaji
Agricultural Council of Tanzania
S.L.P 14130, Dar es Salaam.

**Simu:** (+255) 719260726

**Barua pepe:** act@actanzania.or.tz

MembershipComm@actanzania.or.tz

**Tovuti:** www.actanzania.or.tz

## Malengo ya ACT

- Kujenga mazingira wezeshi kwa kilimo-biashara
- Kujengea uwezo wanachama wa ACT katika utoaji wa huduma
- Kutuma na kupokea taarifa kutoka kwa wanachama na wadau wengine zinazohusu ustawi wa sekta ya kilimo nchini.
- Kuratibu na kuendesha mashirikiano katika ngazi ya taifa na wilaya
- Kuratibu jitihada za sekta ya umma na binafsi katika uenddelezaji wa kilimo-biashara

## Hii Ndiyo PFS

Ubia wa mradi wa PFS unaratibu na kuwezesha watendaji mbalimbali kwenye mnyororo wa thamani wa wadau chini ya mfumo wa mashirikiano kati ya sekta ya Umma na Binafsi (PPP). Mradi unatekelezwa na Baraza la Kilimo Tanzania. Lengo lake ni kuchangia na kuongeza kiwango cha mafanikio yaliyopatikana kwenye awamu ya pili ya Mradi wa Ubia wa Kilimo Tanzania (TAP2) katika kipindi cha Oktoba 2014 hadi Mei 2020. Mradi huo ulifanikiwa ukuaji wa kilimo kwa kutumia mbinu za kilimo-biashara na uwekezaji.

### MalengoyaMradi

**Lengo kuu ni;** Kuongeza usalama wa chakula na lishe, nakupunguza umasikini. Umaskini unatarajiwa kupungua kwa 17%, halikadhalika na ukosefu walishe kwa Watoto kupungua kwa 5%.

### Utaratibu wa utekelezaji

Mradi utatumia mbinu ya ubia katika utekelezaji wa mradi. Mradi wa PFS, chini ya Baraza la kilimo Tanzania (ACT). Utaratibu na kuongeza uwezeshaji na utekelezaji ili kuhakikisha ubia unahimarishwa na mafanikio tarajiwa yanafanikiwa. Mradi unatumia ujuzi na maarifa ili kutatua vikwazo muhimu kwenye mnyororo wa thamani. Mradi umeainisha asasi za kiraia 35, wabia kutoka sekta ya umma na binafsi (ndani na nje ya nchi), wenye uwezo na majukumu mbalimbali watakao shirikishwa katika kazi ya ubia.

**Akaunti za Mitandao ya Kijamii:**

LinkedIn @barazalakilimo

Twitter @act_tz

Instagram barazalakilimotanzania

Facebook Agricultural Council of Tanzania

***PFS inawajibika kwa Bodi ya Wakurugenziwa ACT***